**KARATASI 102/2**
**KIDATO CHA NNE**
**IDARA YA KISWAHILI**
**SARUFI NA MATUMIZI YA LUGHA**
**MTIHANI WA KABLA YA MWIGO**
**MUHULA WA PILI 2019**
**SAA: 2 ½**

**JINA: ………………………………………………...NAMBA YAKO:………………………**

**SAHIHI YA MTAHINIWA …………....**

**TAREHE …………………………………**

**DARASA ………………………………….**

**Maagizo:**

**Jibu maswali <u>yote</u>. Majibu yako yaandikwe katika nafasi ulizoachiwa.**

| SWALI | UPEO | ALAMA |
|---|---|---|
| UFAHAMU | 15 | |
| UFUPISHO | 15 | |
| SARUFI | 40 | |
| ISIMU JAMII | 10 | |
| JUMLA | 80 | |

**UFAHAMU (ALAMA 15)**

**Soma kifungu kifuatacho kasha ujibu maswali.**

Suala la mahusiano ya wanadamu katika jamii, uainishaji wake na uathihirikaji wake limewashughulisha wataalamu wa elimu jamii kwa dahari ya miaka. Suala hili huwatafakarisha wataalamu hao kutokana na umuhimu wake katika maisha ya binadamu msingi mkuu wa uainishaji wa mahusiano hayo ni kukichunguza kipindi cha mahusiano yenyewe. Yapo mahusiano baina ya waja ambayo yanachukua muda mfupi, kwa mfano saa au dakika chache, na mengine ambayo huenda yakachukua miaka ayami.

Mahusiano ya muda mrefu kabisa ni yale yanayojulikana kama mahusiano ya kudumu. Inamkinika kudai kuwa miundo ya kijamii, kisiasa na kiuchumi huweza kuyadhibiti mahusiano hayo kwa kiasi kikubwa. Watu wengi huitikadi kuwa uhusiano uliopo baina ya mtu na jamaa yake utachukua muda mrefu, na kwa hivyo ni uhusiano wa kudumu. Hali hii hutokana na uhalisi kuwa tunahusiana na jamaa zetu kwa kipindi kirefu labda tangu ukembe hadi utu uzima wetu. Uhusiano huu hautarajiwi kuvunjwa na umbali wa masafa baina yetu; tunaendelea kuwasiliana kwa barua au, katika enzi hii ya utandawazi, kwa kutumia nyenzo za teknohama kama mtandao na simu za mkononi, na kudumisha uhusiano wetu wa kijamaa. Hata hivyo, inawezekena baadhi ya mahusiano ya kijamaa yasiwe ya kudumu. Mathalan, uhusiano uliopo baina ya mke na mume, na ambao unatarajiwa kuwa wa kudumu au kipindi kirefu, unaweza kuvunjwa kwa kutokea kwa talaka. Talaka hiyo inavunja ule uwezekano wa uhusiano wa kudumu unaofumbatwa na sitiari ya pingu za maisha.

Katika ngazi ya pili, mahusiano ya koindi cha wastani, kuna mahusiano yanayohusisha marafiki zetu maishani, shuleni au kwenye taasisi zozote zile, majirani zetu, wenzetu katika mwahali mwa kazi, washirika kwenye sehemu za ibada au za burudani na wenzetu kwenye vyama tofauti na makundi ya kujitolea. Inawezekana kudahili kuwa baadhi ya mahusiano haya, hususan baina ya marafiki na majirani huweza kuwa ya miongo na daima. Hali hii huweza kutegemea muundo na mfano wa jamii. Kwa mfano, kwa majirani wanaoishi kwenye janibu, fulani mahususi, na kwa miaka tawili bila ya kuhajiri. Uhusiano wao na majirani huweza kuwa wa kudumu. Hali hii **inasigana** na hali iliyoko kwenye maisha ya mijini. Maisha ya mijini yana sifa ya kubadilkikabadilika. Isitoshe, kutokana na mfumo wa maisha ya kibepari **yameghoshi** ubinafsi mwingi. Mawimbi ya mabadiliko na ubinafsi uweza kuumomonyoa ukuta wa uhusiano wa kudumu.

Mwelekeo wa maisha ya siku hizi ya uhamaji kutoka maeneo au viambo walikoishi watu unasababisha kupombojea kwa mahusiano ya kudumu baina yao na majirani zao. Uhusiano kati ya wenza katika mazingira ya kazi unahusiana kwa kiasi fulani na ule wa majirani. Vimbunga vya ufutwaji kazi, ubadilishaji wa kazi, hali zisizotegemewa na mifumo ya kimataifa pamoja na hata mifumo ya kisiasa huweza kuathiri mshikamano wa wanaohusika kazini.

Kiwango cha mwisho cha mahusiano ni uhusiano wa mpito au wa muda mfupi. Mahusiano ya aina hii hujiri katika muktadha ambapo pana huduma fulani. Huduma hizi zinaweza kuwa dukani, kwenye sehemu za ibada, kwenye kituo cha mafuta, kwa kinyozi, kwa msusi na kadhalika. Kuna sababu kadha zinazotufanya kuyazungumzia mahusiano ya aina hii kama ya mapito. Kwanza, uwezekano wa mabadiliko ya anayeitoa huduma hiyo ni mkubwa. Si ajabu kuwa unaporudi kwa kinyozi au msusi untambua aliyekushughulikia hayupo. Hata hivyo, kuna **vighairi** hususa pale ambapo mtoa huduma anayehusika ni yule mmoja.

Mahusiano ya mpito yanatawaliwa na "uhusiano wa chembe chembe". Uhusiano wa chembe chembe, bidhaa ya mfumo wa kibepari, unamaanisha kuwa kinachomshughulisha mtu ni chembe ndogo tu ya mwenzake. Chembe hiyo inaweza kuwa huduma, kwa mfano, gazeti analokuuzia mtu, kiatu anachokushonea, nguo anazokufulia, ususi anaokufanyia n.k. Mahusiano ya aina hii yametovukwa na hisia za utu na ni zao la mifumo ya kisasa na kiuchumi na kijamii. Mtu anayehusiana na mwenzake kwa misingi ya chembe ndogo tu, huenda asijali kama mwezake amekosa chakula, amefutwa kazi, amefiliwa na kadhalika.

Suala kuu tunalopaswa kujiuliza nji: Je, tunahusiana vipi na jamaa zetu, taasisi zetu, marafiki zetu na majirani zetu? Je, uhusiano wetu na raia wenzetu ni w aaina gani? Je, uhusiano wetu na nchi yetu ni wa mpito au ni wa kudumu?

(a) Taja kigezo muhimu cha kuzungumzia mahusiano. (al 1)

……………………………………………………………………………………………..

……………………………………………………………………………………………..

(b) Eleza imani ya watu kuhusu uhusiano baina ya jamaa. (al 1)

……………………………………………………………………………………………..

……………………………………………………………………………………………..

(c) Fafanua athari ya technolojia kwenye mahusiano ya watu. (al 2)

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

(d) Eleza sababu nne kuu za kuharibika kwa mahusiano katika maisha ya leo. (al 4)

……………………………………………………………………………………………..

……………………………………………………………………………………………..

……………………………………………………………………………………………..

……………………………………………………………………………………………..

……………………………………………………………………………………………..

……………………………………………………………………………………………..

(e) Taja sifa kuu ya mahusiano ya muda mfupi. (al 2)

……………………………………………………………………………………………..

(f) Je, kifungu hiki kina ujumbe gani mkuu? (al 2)

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………..

……………………………………………………………………………………………..

(g) Eleza maana ya maneno yafutayo kama yalivyotumiwa katika kifungu. (al 3)

(i) inasigana……………………………………………………………………………………

(ii) yameghoshi…………………………………………………………………………………

(iii)vighairi……………………………………………………………………………………..

**UFUPISHO (ALAMA 15)**

Ujambazi wa kimataifa ni tatizo lililowasumbua walimwengu kwa muda mrefu sana. Serikali nyingi zimetumia mapesa mengi kwa miaka mingi sana zikijitahidi kupambana na janga hili. Hata hivyo, fanaka haijapatikana, wala haielekei kamwe kuwa itapatikana leo au karne nyingi baadaye.

Yumkini tatizo kubwa lililopo ni kuhusu jelezi la dhanaya "ujambazi" tena "wa kimataifa". Hili ni tatizo mojawapo na yapo mengi sana. Tatizo la pili ni kiburi. Kuna wale watu binafsi na hasa viongozi w anchi kubwakubwa na serikali zao zilizojiaminisha kuwa ujambaz ni balaa kweli, tena belua, lakini huo ni wa huko, wala hauwezi kuwagusa licha ya kuwashtua wao.

Kulingana na maoni watakaburi hao, ujambazi ni wa watu 'washenzi' wasiostaarabika, wapatikanao katika nchi zisizoendelea bado. Ujambazi peke wanaouona unafaa kukabiliwa ni dhidi ya mbubujiko wa madawa ya kulevya uliosababishwa na vinyagarika kutoka nchi hizo maaluni za "ulimwengu wa tatu". Kulingana na wastaarabu wa nchi zilizoendelea, vinyangarika hivi ndivyo hasa adui mkubwa wa ustaarabu ulimwenguni na ni sharti vifagiliwe mbali bila huruma. Baada ya kusawasagwa, ulimwengu mstaarabu utazidi kutononoka na ahadi ya mbingu hapa ardhini itakamilika.

Imani ya watu hawa ya kuwa ujambazi wa kimataifa, hata iwapo upo, hauwezi kuwashtua wala kuwatingisha wao ilikuwa kamili na timamu. Ilikuwa kamili na timamu hadi hapo mwezi Septemba tarehe 11 mwaka wa 2001, ndege tatu za abiria zilipoelekezwa katika majumba mawili ya fahari, yenye urefu wa zaidi ya ghorofa mia moja na kuyatwangilia mbali. Mshtuko na kimako! Kimako kwa kuwa, kabla ya siku hiyo, Wamarekani hawangeweza kudhani kwamba ingewezekana taifa lolote au mtu yeyote kuthubutu kushambulia nchi yao, taifa wasifa lililojihami barabara dhidi ya aina yoyote ile ya uchokozi kutoka pembe lo lote la dunia.

Hakuna ulimwenguni mzima, aliyeamini kuwa Marekani ingeweza kushambuliwa. Kwa ajili hiyo, mshtuko uliitingisha ardhi yote na huzuni ilitanda kote, kama kwamba sayari nzima imeshambuliwa, wala sio Marekani pekee.

Mintarafu hiyo, Marekani ilipolipiza kisasi kwa kuwaunguza waliokuwemo na wasiokuwemo kwa mabomu hatari huko Afghanistan, idadi kubwa ya watu duniani ilishangilia na kusherehekea. Kwa bahati mbaya, tafsiri ya shambulizi la minara-pacha na Newyork na lile la Pentagon, uti wa uwezo wa kivita wa Marekani, ulizorota. Kuna wengi waliodhani huo ni mwanzo wa vita vya Waislamu dhidi ya Wakristo na kwa muda, Waislamu wote wakashukiwa kimakosa kuwa ni majambazi wa kimataifa.

(a) Bila kubadilisha maana, fupisha aya tatu za kwanza. (maneno 65 – 75) (al 10, 2 za utiririko)

Matayarisho

………………………………………………………………………………………………..

………………………………………………………………………………………………..

………………………………………………………………………………………………..

………………………………………………………………………………………………..

………………………………………………………………………………………………..

………………………………………………………………………………………………..

………………………………………………………………………………………………..

………………………………………………………………………………………………..

Nakala safi

………………………………………………………………………………………………..

………………………………………………………………………………………………..

………………………………………………………………………………………………..

………………………………………………………………………………………………..

………………………………………………………………………………………………..

………………………………………………………………………………………………..

………………………………………………………………………………………………..

………………………………………………………………………………………………..

(b) Ukizingatia aya tatu za mwisho, fafanua fikira za watu na mambo yote yaliyotokea baada ya Septemba tarehe 11, 2001. (maneno 65 – 75) (al 10, 2 za utiririko)

Matayarisho

………………………………………………………………………………………………..

………………………………………………………………………………………………..

………………………………………………………………………………………………..

………………………………………………………………………………………………..

………………………………………………………………………………………………..

………………………………………………………………………………………………..

………………………………………………………………………………………………..

………………………………………………………………………………………………..

Nakala safi

……………………………………………………………………………………………..

……………………………………………………………………………………………..

……………………………………………………………………………………………..

……………………………………………………………………………………………..

……………………………………………………………………………………………..

……………………………………………………………………………………………..

……………………………………………………………………………………………..

……………………………………………………………………………………………..

**MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 40)**

(a) Silabi ni nini? (al 2)

……………………………………………………………………………………………..

……………………………………………………………………………………………..

……………………………………………………………………………………………..

(b) Tenga silabi katika maneno yafuatayo kisha uandike aina yake. (al 2)

(i) igwa

……………………………………………………………………………………………..

……………………………………………………………………………………………..

(ii) Oa

……………………………………………………………………………………………..

……………………………………………………………………………………………..

(c) Dhihirisha panapotiwa shadda katika maneno yafuatayo. (al 2)

(i) Galagala …………………………………………………………………………………

(ii) Teketeza ………………………………………………………………………………...

(d) Bainisha nomino katika sentensi zifuatazo kisha utaje aina zake. (al 2)

(i) Uhubiri wa mama huyu una mvuto mkubwa

…………………………………………………………………………………………….

……………………………………………………………………………………………..

……………………………………………………………………………………………..

(ii) Kabati hili limevamiwa na wadudu wengi waharibifu.

…………………………………………………………………………………………………..

…………………………………………………………………………………………………..

…………………………………………………………………………………………………..

(e) Eleza matumizi ya kihusishi kwa katika sentensi ifuatayo. (al 2)

Tahadhari huandikwa kwa hati nzito.

…………………………………………………………………………………………………..

…………………………………………………………………………………………………..

(f) Tenga viambishi na mzizi katika neno lifuatalo. (al 2)

Siji.

…………………………………………………………………………………………………..

…………………………………………………………………………………………………..

(g) Unda nomino kutokana na kivumishi kifatacho. (al 1)

Tepetevu

…………………………………………………………………………………………………..

(h) Pigia mstari na kuainisha kirai katika sentensi ifuatayo. (al 2)

Haifai kujenga karubu na nyaya za umeme

…………………………………………………………………………………………………..

…………………………………………………………………………………………………..

(i) Bainisha shamirisho kitondo katika sentensi ifuatayo. (al 2)

Mzalendo amemwandikia mhariri barua.

…………………………………………………………………………………………………..

…………………………………………………………………………………………………..

…………………………………………………………………………………………………..

(j) Eleza kama sentensi ifuatayo ni sahili, ambatano ama changamano. (al 2)

Tulipewa ratiba ya shughuli hiyo lakini hatukuitia maanani

…………………………………………………………………………………………………..

…………………………………………………………………………………………………..

…………………………………………………………………………………………………..

(k) Bainisha vishazi huru na vishazi tegemezi katika sentensi ifuatayo. (al 2)

Simu tamba ambayo ameninunulia imenirahisishia mawasiliano

…………………………………………………………………………………………………..

…………………………………………………………………………………………………..

…………………………………………………………………………………………………..

…………………………………………………………………………………………………..

(l) Kanusha sentensi ifuatayo. (al 2)

Ninamtarajia mpwa wangu awasili leo

…………………………………………………………………………………………………..

…………………………………………………………………………………………………..

(m) Andika katika wingi. (al 2)

Huzuni aliyokuwa nayo yatima huyu ilinitia kite na imani.

…………………………………………………………………………………………………..

…………………………………………………………………………………………………..

…………………………………………………………………………………………………..

(n) Andika kinyume cha neno lililopigwa mstari. (al 1)

Mhalifu huyu alitunga mimba

…………………………………………………………………………………………………..

…………………………………………………………………………………………………..

(o) Bainisha matumizi ya **KI** katika sentensi ifautayo. (al 1)

Jua limekuwa likiwaka tangu Januari

…………………………………………………………………………………………………..

…………………………………………………………………………………………………..

(p) Bainisha matumizi ya **ka** katika sentensi ifuatayo: (al 1)

Sungura alifika nyumbani akamsalimu mkewe, akafululiza msalani akaoga

…………………………………………………………………………………………………..

…………………………………………………………………………………………………..

(q) Akifisha sentensi hii: (al 2)

Mmea wa pareto ni muhimu mno nchini akasema afisa wa kilimo

…………………………………………………………………………………………………..

…………………………………………………………………………………………………..

(r) Badilisha katika usemi wa taarifa: (al 2)

"Tutakusaidia ikiwa utashirikiana nasi," afisa wa usalama akasem.

……………………………………………………………………………………………..

……………………………………………………………………………………………..

……………………………………………………………………………………………..

(s) Andika katika ukubwa ukizingatia neno lililopigwa mstari. (al 1)

Aliyerembesha <u>uso</u> kwa poda.

……………………………………………………………………………………………..

……………………………………………………………………………………………..

(t) Bainisha maana mbalimbali za sentensi ifuatayo: (al 3)

Mwalimu amempigia wanafunzi simu

……………………………………………………………………………………………..

……………………………………………………………………………………………..

……………………………………………………………………………………………..

……………………………………………………………………………………………..

……………………………………………………………………………………………..

……………………………………………………………………………………………..

(u) Silabi mwambatano ni nini? (al 1)

……………………………………………………………………………………………..

(v) Tunga sentensi moja udhihirishe maana mbili za neno hili: <u>Rudi</u> (al 1)

……………………………………………………………………………………………..

……………………………………………………………………………………………..

…………………………………………………………………………………………….

(w) Pigia mstari vivumishi katika sentensi ifuatayo kisha uandike aina yake. (al 2)

Bibi huyu ni mpole uso wake wenye haya huuinamisha kila mara.

……………………………………………………………………………………………..

……………………………………………………………………………………………..

……………………………………………………………………………………………..

**ISIMU JAMII**

Maenezi ya Kiswahili Afrika mashariki punde baada ya uhuru yalikuwa na chagamoto tele. Fafanua zozote tano. (al 10)